# MIRADI ILIYOPITIWA NA MBIO ZA MWENGE 2025

### 1. MABWENI MAWILI KATIKA SHULE YA SEKONDARI KYAKA

Mradi una thamani ya shilingi 260,000,000.00 kutoka Serikali kuu kupitia programu ya SEQUIP kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita. Mradi huu ulianza kutekelezwa tarehe 15/03/2025 kwa njia ya "Force account" ambapo manunuzi yote yalifanyika kupitia mfumo wa Nest na kukamilika tarehe 20/08/2025.

Kazi kubwa zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa majengo mawili na kuweka vitanda themanini 80 vyenye uwezo wa kulaza wanafunzi 160. Mradi huu unatarajiwa kutoa nafasi ya kudahili wanafunzi 80 wa kidato cha tano kwa mwaka 2026/2027 kutoka maeneo mbalimbali nchini.





### 2. NYUMBA MOJA YENYE UWEZO WA KUKAA FAMILIA TATU KATIKA ZAHANATI YA KASHABA

Thamani ya mradi huu ni shilingi 104,991,627.58 ambapo Halmashauri kupitia mapato yake ya ndani imechangia Tsh 100,000,000.00 na jamii imechangia Tsh 4,991,627.58.

Mradi huu umetekelezwa kwa njia ya manunuzi ya "Force Account" kupitia mfumo wa NeST na ulianza kutekelezwa tarehe 16/03/2025 na kukamilika 15/08/2025 Mradi huu umekamilika na upo tayari.



HALMASHAURI YA WILAYA MISSENYI

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI

# MWENGE WA UHURU MWAKA 2025





**MHE. KANALI (MST) HAMIS MAIGA**
**MKUU WA WILAYA YA MISSENYI**

**Karibu Mwenge wa Uhuru 2025 katia Wilaya ya Missenyi, Mwenge wa Uhuru ukiwa Wilaya ya Missenyi umekimbizwa kwa kilomita 65 na kutembelea, kuzindua na kukagua mirdi saba yenye thamani ya shilingi bilioni 2.4**

## AHSANTENI KWA KUJITOKEZA !!

**KAULI MBIU**

**"Jitokeze Kushiriki Uchaguzi Mkuu kwa Amani na Utulivu"**

### 3. MRADI WA USTAWISHAJI NA UGAWAJI WA MICHE YA KAHAWA KWA WAKULIMA.

Mradi huu umegharimu Tsh. 135,000,000.00 kutoka mapato ya ndani ambazo zimetumika kununua miche 450,000 inayogawiwa kwa wakulima 1,671 katika kata zote 20 za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi.



Usambazaji wa miche ya kahawa kwa wakulima ulianza mwaka 2020/2021 katika kutekeleza Mkakati wa Taifa wa kuendeleza zao la kahawa 2021-2025. Hadi sasa wakulima 2,856 wamenufaika na miche 1,682,557 aina ya Robusta ikiwa 90.4% na Arabica 9.6%. Miche hii imepandwa katika ekari 3,516 na uzalishaji unaendelea.

Uzalishaji wa kahawa umeongezeka kutoka wastani wa Tani 1,137 kwa mwaka 2020/2021 hadi Tani 2,033.5 kwa mwaka 2024/2025 na kupelekea kuongezeka kwa ushuru wa kahawa kutoka Tsh.37,000,000.00 hadi Tsh 276,480,813.00 Kwa mwaka 2025/2026, miche 3,210,000 itasambazwa kwa wakulima 5,000 na kupandwa kwenye ekari 7,229 ikiwa miche 450,000 imetokana na Halmashauri na miche 2,760,000 ni mchango kutoka kwa wadau.

### 4. ENEO LINALOTARAJIWA KUJENGWA UWANJA WA MICHEZO WENYE MAJUKWAA.

Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi katika kutekeleza sera ya Michezo ya Taifa imetwaa eneo lenye ukubwa wa mita za Mraba 83,061 kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wenye majukwaa.

Kwa mwaka wa fedha 2025/26 Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi ilitenga Tsh. 270,000,000/= katika mapato ya ndani kwa ajili ya fidia ya wananchi.

Uthamini wa fidia ulianza tarehe 23/05/2025 na kukamilika 31/07/2025 na thamani ya fidia stahiki ni Tsh. 236,712,150.00. Tayari waguswa wameshalipwa fidia zao.



### 5. MRADI WA UJENZI WA WODI YA WAGONJWA BINAFSI KATIKA KITUO CHA AFYA BUNAZI

Mradi huu ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 03/05/2024 na kukamilika tarehe 05/10/2024 kwa njia ya manunuzi ya "Force Account "kupitia mfumo wa manunuzi Serikalini NeST. Mradi huu una thamani ya Tsh. 126,993,000.00 ambapo kiasi cha Tsh 120,000,000.00 zimetoka mapato ya ndani na kiasi cha Tshs. 6,993,000.00 zimetoka katika michango ya Mwenge. Mradi huu umekamilika na unatumika.



### 6. KIKUNDI CHA MISSENYI NUTRITIONAL FLOUR GROUP

Kikundi cha Missenyi Nutritional Flour Group kimewezeshwa Tsh 64,000,000.00 kutoka mapato ya ndani zilizotumika kununua na kufunga mashine ya kusaga na kukoboa, kununua malighafi na shughuli za uendeshaji. Kikundi hiki kinazalisha unga wa lishe, Dona na Sembe, ambapo mfuko wa unga wa lishe wa kilo 25 unauzwa Tsh.57,500.00 na unga wa sembe wa kilo 25 unauzwa Tsh.40,000.00 na unga wa Dona kilo 25 unauzwa Tsh.20,000.00.



### 7. MRADI WA UBORESHAJI WA HUDUMA YA MAJI KATIKA ENEO LA MUTUKULA

Mradi huu unatekelezwa na mkandarasi ESTATE CONTRACTOR CO. LTD kutoka DODOMA kwa gharama ya Tshs.1,491,324,622.28 kati ya fedha hizo Tshs.1,489,074,622.28 ni fedha toka Serikali Kuu na Tshs.2,250,000.00 nguvu za wananchi. Shughuli zinazofanyika ni Ujenzi wa tenki la ujazo wa lita 100,000, mnara wa urefu wa mita 12 kwaajili ya kubeba tenki la lita 150,000, nyumba ya mitambo, uzio wa eneo la mradi, Ununuzi na ufungaji wa pump mbili , piki nne na gari moja aina ya Toyota, Ujenzi wa ofisi ya BUWASA Mutukula,uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa bomba kilomita 14. Mpaka sasa mradi umefikia asilimia 70 ya utekelezaji.



